



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI MBEYA



Kumb. Na: MCC/PHD/K.20/VOL/17

TAREHE 27/09 /2021

Wananchi Wote,
Halmashauri ya Jiji la Mbeya

TANGAZO LA KUMPATA FUNDI JAMII

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

2. Halmashauri ya Jiji la Mbeya inawatangazia Wananchi wa Jiji la Mbeya wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi ya ujenzi wa majengo katika Kata ya Ilemi kuomba kazi ya Ujenzi kama **FUNDI JAMII** kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Ilemi itakayojengwa katika Kata ya Ilemi mtaa wa Masewe.
3. Majengo yatakayojengwa ni kama ifuatavyo;
 - i) Jengo la wagonjwa wa nje (OPD)
 - ii) Jengo la wodi ya wazazi
 - iii) Jengo la Upasuaji
 - iv) Ujenzi wa choo na mashimo(Septic na soakway PIT)
 - v) Jengo la kufulia
 - vi) Kichomea taka
4. Mwombaji anatakiwa awe na sifa zifuatazo;
 - a) Awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu (3) wa ujenzi wa majengo ya Serikali.
 - b) Awe na vifaa vya msingi katika masuala ya ujenzi.
 - c) Awe na ujuzi wa kutosha na uwezo wa kusoma ramani za majengo ya Serikali.
 - d) Awe na fedha/mtaji wa kuanzia kwa ajili ya kuwalipa vibarua atakaowaajiri vilevile awe na Akaunti ya Benki
 - e) Awe na uwezo wa kufanya kazi kuanzia hatua ya awali hadi umaliziaji.
5. Mwombaji mwenye nia na sifa anakaribishwa kuchukuwa **FOMU YA MAOMBI** na kupata maelezo kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Jiji S.L.P. 149, Mbeya. Ofisi ipo ghorofa ya kwanza katika Makao Makuu ya Ofisi za Halmashauri ya Jiji, sambamba na Maktaba ya Mkoa, Mkabala na Ofisi za Posta Mbeya, Chumba Na 107. Ofisi iko wazi kuanzia **saa 1.30 asubuhi mpaka saa 9:30 Alasiri** Jumatatu mpaka Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu. **Fomu za maombi zinatolewa bure.**
6. Mwombaji anatakiwa kuomba kazi ya kujenga Jengo moja tu.

7. Maombi yataendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi Na.7 ya mwaka 2011 na Kanuni zake ya mwaka 2013 Tangazo la Serikali Na.446
8. Mwombaji mwenye nia na uwezo anaweza kufanya ziara ya kutembelea eneo la mradi. Ziara ya kutembelea eneo la mradi itafanyika **tarehe 28/09/2021**, kuanzia saa 3:00 asubuhi kwa gharama zake ili kutambua na kujiridhisha eneo la mradi pamoja na masuala mengine yatakayohitaji ufafanuzi wa Halmashauri. Wataalamu wa Halmashauri watakuwepo eneo la mradi.
9. Maombi yote yawasilishwe kwa katibu wa Bodi ya zabuni yakiwa ndani ya bahasha iliyofungwa ipasavyo Bahasha zenye maombi zionyeshe kazi unayoomba kwa upande mmoja na kuelekezwa kwa anuani ifuatavyo;

**Katibu wa Bodi ya zabuni
Halmashauri ya Jiji la Mbeya
S.L.P 149
MBEYA**

- 10 Mwisho wa kupokea maombi hayo ni siku ya Alhamis **tarehe 30/09/2021** saa 4.00 Asubuhi. Waombaji au wawakilishi wote wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa maombi hayo utakaofanyika **tarehe 30/09/2021** katika ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya.
- 11 Maombi yatakayochelewa kupokelewa hayatafunguliwa.

J. Haule

Upendo J. Haule
**KAIMU MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI- MBEYA**

**K. N. Y. MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI
MBEYA**